# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS,
## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO

**Kumb. Na. AB.113/388/94** **31 May 2022**

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo kupitia Kibali cha Idhini ya kutekeleza Ikama na Bajeti kwa Ajira Mpya katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 chenye **Kumb. Na.** FA.97/228/01/9 cha tarehe 13 Mei, 2022 kilichotolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (UTUMISHI) anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi **Nne (04)** kama ilivyoainishwa katika tangazo hili.

### 1.0 KATIBU MUHTASI DARAJA III (PERSONAL SECRETARY III) - NAFASI 2

### 1.1 SIFA ZA MUOMBAJI

i. Awe muhitimu wa Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI)
ii. Awe amehudhuria mafunzo ya Uhazili na kufaulu Mtihani wa hatua ya tatu.
iii. Awe amefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika moja.
iv. Awe amepata mafunzo ya kompyuta kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika program za Windows, Microsoft Office, Internet, E-Mail na Publisher.

### 1.2 MAJUKUMU YA KAZI

i. Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida.
ii. Kusaidia kupokea wageni na kuwasaidia shida zao na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
iii. Kusaidia kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio, miradi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa katika Ofisi anayofanyia kazi, na kumuarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika.
iv. Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo ofisini.
v. Kusaidia kufikisha maelekezo ya Mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake na kumuarifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizi hao.
vi. Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa Maofisa walio katika sehemu alipo, na kuyakusanya , kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.
vii. Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na Msimamizi wake wakazi.

### 1.3 NGAZI YA MSHAHARA

- Mwombaji atakaefanikiwa kuajiriwa kwa Cheo cha Katibu Muhtasi Daraja la III atalipwa mshahara ngazi ya TGS B/1 kwa mwezi.

## 1.0 DEREVA DARAJA II (DRIVER II) - NAFASI 2

### 2.1 SIFA ZA MUOMBAJI

i. Awe na cheti cha kidato cha Nne (IV) au cha Sita (VI).
ii. Leseni la Daraja la E au C1 ya uendeshaji Magari ambayo imefanyiwa kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila ya kusababisha ajali.
iii. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi stadi (VETA) au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.
iv. Waombaji wenye cheti cha majaribio ya Ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza.

### 2.2 MAJUKUMU YA KAZI

i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
iii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari.
iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali.
v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari,
vi. Kufanya usafi wa gari, na
vii. Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na msimamizi wake.

### 2.3 NGAZI YA MSHAHARA

- Mwombaji atakaefanikiwa kuajiriwa kwa Cheo cha Dereva Daraja la II atalipwa mshahara ngazi ya TGS B/1 kwa mwezi.

## 3.0 MASHARTI YA JUMLA

i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri kuanzia miaka 18-45.
ii. Waombaji wote waambatishe nakala ya cheti cha kuzaliwa.
iii. Barua ya muombaji ioneshe anuani anayotumia kwa sasa pamoja na namba za simu ikiambatana na:
    a) Nakala za vyeti vya taaluma,
    b) Nakala za vyeti vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
    c) Maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu zinazopatikana pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
    d) Picha mbili (2) za "**Passport Size**" za hivi karibuni.
    e) **Kitambulisho au namba ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA)**

iv. Waombaji waliowahi kupatikana na kosa la jinai hatafikiriwa.

v. "**Testmonials**", "**Provisional Results**", "**Statement of results**", hati matokeo za kidato cha nne na sita (**FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS**) **HAVITAKUBALIWA**.

vi. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU, NECTA na NACTE).

vii. Waombaji aliyestaafishwa/kuachishwa kazi katika Utumishi wa Umma haruhusiwi kuomba isipokuwa kama ana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.

**viii. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.**

Waombaji wenye sifa wanatakiwa kuwasilisha maombi yao katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo au kutuma maombi kupitia Posta kwa anuani ifuatayo;-

**Mkurugenzi wa Manispaa,**
**Manispaa ya Ubungo,**
**S.L.P 55068,**
**DAR ES SALAAM.**

**Mwisho wa kupokea maombi ya kazi ni tarehe 15 Juni, 2022 saa tisa na nusu alasiri.**

NB: Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Halmashauri www.ubungomc.go.tz

Beatrice R. Dominic
**MKURUGENZI WA MANISPAA**

MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO
DAR-ES-SALAAM

Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa. Luguruni, Barabara ya Morogoro, S.L.P: 55068, Dar es Salaam,
Unaweza pia kuwasiliana nasi kwa Simu. 0222-926341, Nukushi: 0222-92342, Tovuti; www. ubungomc.go.tz,
Barua pepe; info@ubungomc.go.tz

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

*Jiandae kuhesabiwa siku ya Jumanne tarehe 23 Agosti, 2022.*